MACHI MMXXIV-TOLEO LA XXX

# NGURUMO

*ya mwandishi*



LAURA PETTIE

# Siginecha

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— SIGINECHA —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— TATU KIONDO— Uk 03

**New In Town:** NIFANYEJE BIASHARA MTANDAONI **—** uk 04

**PITIO LA VITABU**— DIWANI YA KIMBUNGA '2'—Uk 06

**MAKALA— SAIKOLOJIA**: WAZA MAWAZO CHANYA—Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji '15'— uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '05'— Uk 10

**Sako kwa Bako– Patrick Nkika:** MWALIMU MWENYE ROHO YA VITABU **—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '1'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '12'- Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '9'- Uk 16

**HABARI:** ABDULRAZAK GURNAH- Mgeni Rasmi Tuzo ya Nyerere – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Zijue maktaba 10 bora Afrika '1'—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** — RICHEST MAN IN BABYLON—Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO —** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Miaka 62 ya Uhuru : Vituko Vya Uhuru**- '5'-**Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Ukamataji, aupekuzi na Dhamana ya Polisi—Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI: SIGINECHA

Wasalaam,

Nakusalimieni nyote ndani na nje ya Tanzania. Najua mmesubiri kwa hamu jarida letu la mwezi wa Machi kwa kuwa wengine wanataka kuendelea na riwaya walizokwishakuzianza na wengine wanapenda kuwasoma waandishi wao. Yaani kila msomaji analo lile linalomvutia katika jarida hili. Nasi tunasema asante kwa yote.

Mwezi huu nataka nikuulize tu, je; unafahamu nini kuhusu Siginecha (nimetohoa)? Siginecha ni alama ya kimaandishi au yaweza kuwa ya kidole ambayo mtu huiweka kwenye andiko kuthibitisha uhalali wa melezo aliyoyatoa mtu au utambulisho wake kimaandishi.

Lakini kuna aina nyingine ya siginecha ambayo inabeba muktadha uleule wa 'alama'. Lakini hii ni ile alama ambayo mtu anabakisha kwenye mioyo ya wengine au kwenye jamii inayomzunguka, ama kwa kufanya jambo fulani ambalo litagusa mioyo ya watu nk.

Hapa juzijuzi nilikutana na andiko moja kwenye ukuta wa facebook wa mwanadada Bhoke Rose Maseke, mfanyabiashara maarufu sana mtandaoni aliyejinyakulia Tuzo tepe ya Chimbo Bora la biashara kupitia Facebook. Tuzo ambazo zilibuniwa na muasisi wa kurasa na kampuni ya Nyumbani Business Plan LTD Bwana Frank Ndyanabo

Andiko hilo katika aya ya kwanza liliandika hivi "Hadi muda huu Napata shida kumuaminisha Noreen kuwa Laura Pettie ni binadamu halisi sio mchoro na yupo duniani anaishi". Mtoto huyo (Noreem) alikuwa akisoma kitabu 'KIROBA CHEUSI' kilichoandikwa na Laura Pettie.

Binafsi nilitafakari sana hili andiko na nikajiuliza, kwanini huyu Noreen achanganyikiwe kuhusu Laura kama ni binadamu au ni mtu wa kufikirika? Ameacha nini kwenye moyo wa huyu mtoto? Lakini niliposoma hoja za watu waliosoma andiko lile, niligundua kuwa wengi wanaosoma vitabu vya Laura au maandiko yake mtandaoni, wapo ambao wanatamani hata kumgusa, au kupiga naye picha mwanadada huyo.

Hii ni siginecha. Siginecha iliyo au inayobaki mioyoni mwa watu. Huyu mtoto (Noreen) haamini kama Laura ni mtu kweli. Je wewe kwa kile unachofanya, unaacha alama gani katika jamii?

Katika toleo lijalo tutahakikisha Laura Pettie anapatikana jaridani ili tumweke ulingoni kama yeye mwenyewe afanyavyo kwa wengine kwenye ukuta wake wa Facebook.

Nakutakieni, Eid Mubarak njema kwenu nyote.

***Richard Mwambe—30 March, 2024***

# MWANDISHI WETU: TATU KIONDO

Naitwa Tatu Kiondo, nimezaliwa mkoa wa Dar es Salaam. Kwa sasa ninaisha Ubungo.

Historia yangu katika utunzi na uandishi wa Hadithi ilianzia nikiwa mdogo wakati nilipokua shule ya msingi. Nakumbuka darasa la nne nilianza kuandika hadithi kutumia michoro kwenye daftari kisha nawapa wanafunzi wenzangu wanasoma.

Walikua wanagombania sana maana daftari lenyewe linakua moja basi kila mtu akimgoja mwenzie asome kisha ampe nae asome ikawa hivyo mpaka zikawa daftari zangu zinapotea kwa watu kuazimana.

Nilipoingia sekondari nikawa naendelea kuandika ila sio sana sababu nilijikita sana kusoma, nilipenda sana kusoma hadithi kupitia magazeti. Kuna kipindi nilikuwa nakwenda pale posta kwenye jengo la ushirika alipokua anafanya kazi baba yangu mdogo anaitwa Hamisi Mwinyi. Kila nikifika pale lazima anipe gazeti la kiu nikawa nafuatilia hadithi. Badae nikaingia kusoma kwenye vitabu vya waandishi Ben mtobwa, Hammie Rajabu Eric shigongo Patrick massawe na wengine wengi mpaka chombezo za kina ndauka nimezisoma sana.

Safari yangu ya uandishi ilianzia mwaka 2013 kipindi hicho nilikua nafanya kazi kwenye kampuni ya mtu binafsi nikiwa kama secretary, nikapewa laptop ya kazi, nikawa narudi nayo nyumbani basi nikimaliza kazi zangu nikawa naandika hadithi. Niliandika hadithi kama tatu nikawa nazipeleka kwenye magazeti mbalimbali, kuna siku nilipeleka pale global publisher kipindi hicho ofisi zao zilikua Mwenge, nilikutana na kaka Joseph Shaluwa nikamueleza shida yangu akasema nimuachie azipitie. Nikampatia simulizi mbili, kesho yake nikaenda akaniambia zina makosa hivyo natakiwa kuzisahihisha na kuzipangilia upya, nikachukua nikarudi nazo maana niliziprint.

Basi kiu yangu haikuishia hapo nikasema siku moja lazima simulizi zangu zitoke kwenye magazeti yao.

Nikahangaika sehemu nyingine ila na pale Global sikuacha kupeleka maana kulikua na mashindano ya waandishi lakini sikufanikiwa niliishia kwenye kumi bora sikupata nafasi ya kuchaguliwa.
Siku moja nikiwa kazini simu yangu iliingia ujumbe nikaufungua ulitoka kwa kaka Shalua akiniambia “ Tatu mdogo wangu hongera sana nimeona hadithi yako kwenye gazeti la Habari leo” Nilifurahi sana nilimpigia kaka Shaluwa tukaongea kisha nikamshukuru maana nae hakuamini kama nilipeleka sehemu nyingine lakini mwisho wa siku Habari Leo wakanikubali na kuzichapisha.

Mpaka sasa nimefanikiwa kuchapa kitabu kimoja ingawaje nina mpango mwaka huu kutoa kitabu kingine. Nina hadithi tisa ambazo nimeziandika pia uwa ninapost simulizi zangu bure kama burudani kupitia page yangu mpya ya **Simulizi za Tatiana facebook**. Pia **Simulizi club Instagram**.

Kitabu kinapatikana Duka la kona ya Riwaya, na posta kwa George.
Katika waandishi wanaonikosha katika uandishi wao ni Hussein Tuwa, Mzee beka pamoja na Shaluwa wote vitabu vyao ninavyo.
Nawashukuru sana waandishi wenzangu wote kwani tumekua na ushirikiano kwa mambo mbalimbali.

Mwisho kabisa shukrani kwa uongozi wa jarida la NGURUMO YA MWANDISHI Kwa kunipa nafasi hii kuweza kunisoma katika ukurasa huu. Mwenyezi mungu awabariki.


Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini




**Tatu Kiondo… mwandishi wa NAJUA WA KUMPA**

## NEW IN TOWN :
## NIFANYEJE BIASHARA MTANDAONI

Kitabu hiki kinaeleza kwa undani kuhusu namna ya kufanya biashara mitandaoni. Ni kitabu kinachogusa Nyanja nzima ya kuanzia hatua ya kwanza (zero) hadi kupata mafanikio ya juu kibiashara.


Wapo watu wanapenda kufanya biashara mitandaoni lakini hawajui wafanye mbinu gani ili waweze kufanya vizuri. Wapo wajasiriamali ambao wanafanya biashara kwa njia ya mitandao lakini wanakwama baadhi ya maeneo muhimu kupata matunda mazuri yatokanayo na kazi yao. Kimsingi kitabu kinawezesha wafanyabiashara wa mitandaoni kutambua:-

1. Njia za kuwafikia wateja
2. Mbinu za kutumia kutengeneza mvuto kwa wateja
3. Usalama wa mizigo wanayotuma kwa wateja
4. Namna ya kuchagua mtandao bora wa kuuzia na kutangaza bidhaa zao
5. Muda mwafaka wa kuweza kuweka matangazo ya biashara
6. Namna ya kutumia Google Analytics na Facebook Insights na insights za Instagram kuwezesha ukuaji wa biashara yako
7. Mbinu za kuzungumza na wateja waliopanga kununua bidhaa
8. Namna ya kuwasiliana na wateja waliokaa kimya
9. Namna ya kuepuka kufanya biashara ukiwa na stress
10. Umuhimu wa kutunza kumbukumbu za wateja wako kila mara
11. Utayari wa kuwasaidia wateja hata yale yaliyomo nje ya bidhaa zako

Kitabu hiki kimetayarishwa na waandishi wawili, nguli katika biashara kimtandao na waliopata mafanikio kupitia mitandao.

Kinunue, ukisome na ukifanyie kazi. Utawashukuru na utanishukuru baadae.

Bei yake ni 10,000/= tu. Wasiliana na
**Bhoke Rose Maseke kwa 0717-551672**
**Markus Mpangala 0719-226293**



# KITABU: KIMBUNGA (DIWANI) - 2



**JINA LA DIWANI : KIMBUNGA**

**MWANDISHI: HAJI GORA HAJI**

**MWAKA: 1995**

**Katika safu yetu ya Pitio la Vitabu, toleo la 29 tunahama kutoka katika riwaya na kuangazia diwani (ushairi). Basi wale wapenzi wa tanzu ya ushairi, twende pamoja katika kuipitia diwani hii kama tulivoitoa katika mtandao.**

---

Mwandishi anawaomba viongozi wawatetee ili kuepukana na hali hii.Hii ni kutokana na uongozi mbaya ndiyo maana hali kama hii ipo nchini lakini viongozi hawachukui tahadhari yeyote ile.Katika ubeti wa 7,mwandishi anasema;

"Maji yamezidi unga,kwa lodi wa darajani,

Kujitolea mhanga,kwa bei hawezekani,

Mvao wake wa kanga,ni shilingi elifeni,

Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana."

Shairi la "Kibwangai" linajadili dhana ya usaliti wa viongozi wetu kwa wananchi wanaowaongoza. Mwandishi ameonesha jinsi wananchi wanavyowachagua viongozi wao lakini viongozi hao wakishapata madaraka au wakishashika nyazfa wanageuka na kuwasaliti wananchi waliowachagua.Katika ubeti wa 7,msanii anasema;

"Kibwangai lipoona, ni mtu kakamilika,

Akaanza kujivuna,na dharau kuzidiya,

Wala hakujali tena,wenzake walowambiya,

Akahisi hawi nyani,umbo lile litadumu."

Katika Shairi hili manii ametumia taswira ya Kibwangai kuwakilisha viongozi wasaliti na nyani kuwakilisha wananchi wanaoongozwa na akina Kibwangai yaani watawaliwa.

Katika shairi la "Hili Mnatutakiya",mwandishi anaonesha jinsi vyombo vya dola kama vile polisi ,jeshi n.k namna vinavyoshindwa kutekeleza wajibu wake wa kuwalinda raia na kuwashughulikia wahalifu.Katika ubeti wa 1,msanii anasema;

Twasema kinaganaga,tumechoka vumiliya,

Wenzetu mkatubwaga,hasa ukiangaliya,

Hao wezi mwafuga,wazidi kutuibiya,

Hakuna watendewalo,ndipo wakapamba moto.

Msanii ameonesha kuwa vyombo hivyo ndivyo vinavyowalinda wezi,majambazi na matapeli.

Kwa ujumla msanii wa diwani hii anaona kuwa ili tujenge jamii mpya lazima tuwe na uongozi bora unaowajali wananchi wake.


2. Kupiga vita rushwa

Rushwa ni kikwazo kimojawapo kinachokwamisha kujenga jamii kwa upya.Kutokana na rushwa kuota mizizi katika jamii haki hupotea bali wachache wanafaidi matunda ya nchi na wengine wanaendelea kuumia.Katika Shairi la "Rushwa" mwandishi anasema;

"Rushwa kajenga kambi,na kuondoka hataki,

Afanya kila vitimbi,mkaidi hashindiki,

Tumzushiyeni wimbi, isiwe kutuhiliki,




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Tumchimbie handaki,rushwa tukamzikeni."

Katika ubeti huu,mwandishi anatuonesha kuwa lazima jamii yetu ipinge rushwa ili haki na usawa vitawale kwani kupiga vita rushwa ni njia pekee itakayosaidia kujenga jamii mpya ambayo mwandishi ameipendekeza.

3. Umuhimu wa Elimu

Ili tuijenge jamii mpya ni lazima watu wapate elimu na waelimike bila kujali umri wala jinsia.Mwandishi anawahimiza wazee kujiunga na kisomo chenye manufaa ili wafute ujinga wa kutojua kusoma na kuandika.Katika shairi la "Kisomo cha Maarifa" ubeti wa 2, Msanii anasema;

***Itaendelea***

# -SAIKOLOJIA-
## WAZA MAWAZO CHANYA

**Madame Neema Mbilinyi**
**Mgao.**
**Dodoma.**
**Tanzania.**

**+255 763 013 206**



**WAZA MAWAZO CHANYA.**

Habari ya muda huu! Bila shaka u mzima bukheri wa afya ya mwili na akili. Ikiwa unachangamoto yoyote iwe kiafya ama kiakili basi nikusihi kwanza kumshukuru Mungu kwa uhai ulionao hadi saa hii hata umepata uwezo wa kusoma jarida na makala hii. Changamoto ya aina  yoyote ile ipokee, ifanyie tathmini yakinifu, iwekee njia nzuri ya kuitatua. Pili muombe Mungu akuwezeshe kuimaliza changamoto hiyo. Katika makala yetu leo hii tuangazie namna ya kuwaza mawazo chanya. Kwanza tujue maana ya mawazo, mawazo chanya.

**MAWAZO**

- Ni zile fikra mtu alizonazo ambazo hujengwa na matukio yaliyokwisha kutokea.
-Ni zile picha ambazo mtu anakua nazo katika akili yake, iwe picha maneno au picha kama picha halisi lakini alizonazo akilini mwake.
-Mtiririko wa fikra alizonazo mtu katika mfumo wake wa akili iwe ni zilitokana na matukio yaliyokwisha kutokea hapo kabla au ayawazayo na kutamani yatokee.

**MAWAZO CHANYA.**

Ikiwa mawazo ni maana kama hizo nilizokuainishia na yoyote nyingine uliyokaririshiwa basi tuangazie MAWAZO CHANYA. Kumbe kuna MAWAZO CHANYA na MAWAZO HASI. Kumbe tuone maana ya hayo mawazo aina mbili pia.

**i) Mawazo  Chanya**

Mawazo chanya ni yale mawazo yenye kuleta matokeo yenye faida, yaletayo nguvu ya kuvuta mambo mazuri, yaletayo manufaa. Mfano, mtu anawaza kufanya jambo litakaloleta  manufaa iwe kwa watu wengi na hata kwake pia.

**ii) Mawazo Hasi**

Ni yale mawazo au fikra zisizozalisha, hasa hasa ni zile fikra potofu, sio tu kwa muwazaji bali hata kwa wale wamzungukao. Mfano: Wivu wa mapenzi umpelekeao kuua, hasira kupitiliza zinazopelekea kujidhuru, hayo ni matokeo ya mawazo hasi. Nakukumbusha tuu,leo tunazungumzia MAWAZO CHANYA.

Kuanzia huko juu tumeona maana ya mawazo, tukaja kuona aina mbili za mawazo (kwa mujibu wangu mimi), tumeona pia maana zake. Sasa tuone hayo mawazo chanya.
Tunahimizwa na wataalamu wengi wa masuala ya afya ya akili kuwa ni vyema kujiwazia mema, umewahi kujiuliza kwanini? Ngoja leo nikuambie mpenzi wangu.

Ipo faida kubwa sana ya kujiwazia mambo mema, mambo mazuri, mambo kuntu (wa-kileo husema). Kuna faida kubwa sana ya kujiwazia mambo matamu matamu, mazuri mazuri tuu. Haujawahi kusikia, kwamba mambo mengi ya kisaikolojia yanaonekanaga kuwa ni kama uchawi,? Mfano, ile elimu ya kujifanyia MEDITATION, haukuwahi kusikia wasioielewa ile elimu wakiita kuwa ni uchawi? (Sio lengo langu kuzungumzia hilo leo). Basi ile ni moja kati ya elimu ndani ya Saikolojia, ikijumuisha kujifungamanisha katika utulivu wa kuituliza nafsi kwenye uombaji wa kiwango cha juu sana.

Haujawahi kusikia au kuona kwamba wanasaikolojia wengi wakionekana kama watu waliozubaa hivi, yaani sio mcharuko kama akina ndala ndefu, yaani wao huonekana kama washamba fulani, kama watu waliopooza. Unafikiri ni kwanini? Wanawaza mawazo chanya muda wote.
Mawazo chanya. Kuwaza mawazo chanya kuna faida kubwa sana kwa yule anaewaza na kutamka matamshi chanya, kumbukumbu zile tamu zinaporudia katika fikra na ufahamu wake na akathubutu kuzitamka pia basi hujenga nguvu ya kuyavuta yale mazuri anayoyatamani yatokee.  Mfano hai, rafiki yangu mmoja alikua amesimamishwa kazi katika ofisi aliyofanya kazi muda mrefu, walimsimamisha kazi kwa muda usiojulikana. Muda aliokua akikaa nyumbani mara kwa mara alikua akipenda kuutumia kwa kuandika yale anayotamani yatokee kwake. Aliandika

# -SAIKOLOJIA-
## WAZA MAWAZO CHANYA

na kujitamkia mazuri tu. Siku moja akaniambia kuwa muda si mrefu atafungua kampuni ndogo tu awe akiuza maziwa fresh na mayai ya jumla, akaniambia ataajiri vijana si chini ya kumi. Wakati huo anawaza hayo kumbuka ni mtu aliyezoea kuajiriwa, lakini kwa kuwa kwa muda mrefu amekua rafiki hivyo yapo mengi huchota kwangu, ikiwemo na hii ya kuwaza mawazo chanya tuu.

Nilipomuuliza kuwa yupo na kiasi gani cha pesa, aliniambia hana kitu, kwani hata mshahara amesimamishiwa ila sio muda tu hayo anakwenda kuyapata. Nilichomjibu ni kuwa aendelee kuwaza mawazo chanya kwani mawazo chanya huvutia matokeo chanya pia. Nikwambie ni mwaka na miezi kumi tangu aniambie vile, leo hii anamiliki biashara zile alizoniambia. Anauza maziwa fresh, ya mgando, na mayai ya kisasa kwa jumla na rejareja. Kwa siku moja ana uhakika wa kuizungusha biashara yake ambapo wapo vijana 9 wanaoifanya mtaani. Jioni wanaleta hesabu. Kwa mwezi mmoja, anauhakika wa faida yake binafsi kiasi si chini ya milioni moja na laki mbili mpaka milioni moja na laki tatu. Hiyo ni faida yake binafsi. Hapo wafanyakazi ameshawalipa, hivyo hiyo huitumia kama mahitaji yake binafsi kwake na kwa familia kwa ujumla.
Mawazo chanya yamempa kutokea kwa kile alichotamani na mawazo chanya hayo hayo yamempa kuishi vizuri. Mwisho wa mfano.

Nimekupa mfano huo lengo langu ni uione nguvu ya kuwaza mawazo chanya. Ipo nguvu sana Mungu ameiachilia katika mfumo wa akili yako kati ya akili yako na nguvu ya kufanya mambo yatokee. Chunguza hata hivi leo, ukiwaza kwamba huyu mtu mimi namchukia, nikwambie haitokuja kutokea ukampenda, hata ujilazimishe vipi haitokuja kutokea umpende. Na pia kinyume na hivyo, utakuta mtu fulani umempenda sana, basi hata akuudhi namna gani, maadamu umempenda basi utajiambia tu *"kila binadamu na kasoro zake"*. Nazungumzia ile nguvu ya kuwaza mawazo chanya au mawazo hasi.
Unapowaza mawazo yoyote yale ipo nguvu ambayo hufatilizia yale mawazo yako, ukiwaza kushindwa basi utashindwa, ukiwaza kushinda basi utashinda. Haujawahi kujisemea *'nilijua tuu kama itakua hivi'?* Yaani kinatokea kitu ambacho ulikiwazia, basi unajiambia kuwa nilijua kitatokea. Linatokea jambo kwamba ulilifikiria kuwa lingetokea, tena wengine huenda mbali zaidi kwa kuliombea lile jambo walilolifikiria katika fikra zao, kwamba wanaliwazia na kuliombea. Liwe zuri au baya ila maadamu wameliwazia basi moja kwa moja wanatamani litokee. Yaani ni kama umegundua mtu fulani mke au mume wa mtu lakini yuko na mahusiano na mtu mwingine, basi unaanza kuwaza kuwa siku moja watafumaniwa, unaanza na kuombea dua kwa Mungu kuwa watu hao wafumaniwe, watu hao wakifumaniwa hautojisemea *"nilijua tuu"*? Yaani umewaza, iwe hasi au chanya, na dua ukaombea, na inatokea nguvu ya msukumo kweli fumanizi linatokea.

Kuwaza mawazo chanya huvutia uwezekano wa kutokea kwa jambo hilo, hiyo ni nguvu ambayo kila mja amebarikiwa na Muumba wake. Hiyo ni nguvu ya ndani kabisa, hiyo ni tunu ambayo mwanadamu ametunukiwa na Mwenyezi Mungu, Mola mgawa vipaji. Amewapa waja wake uwezo huo. Kila binadamu anao. Basi kumbe kama ni uwezo wa ndani ambao kila mtu amepewa basi ni vyema kujiwazia mambo matamu matamu tu. Jiwazie na kujitamkia mazuri tu. Maisha wakati mwingine yanatuongelesha lugha ngumu sana. Wakati mwingine tunakutana na lugha ngumu kwenye mahusiano ya mapenzi, mahusiano na wale tunaowaamini katika ratiba zetu za kila siku. Lugha ngumu na za kuumiza kwa zile shughuli zetu, hizo tu zitutoshe kutuumiza, na hata hapo pia tusikubari kudumu na maumivu. Tujitamkie mambo mazuri, tujiwazie mawazo chanya.
Wanavyotuwazia vibaya wengine,
Wanavyotuwazia mambo mabaya wengine,
Wanavyotuombea mabaya wengine,
Vyovyote vile wengine wanapotuwazia itoshe hivyo hivyo, tusijiumize na sisi wenyewe kwa kujiwazia mawazo hasi. Vile dunia inavyotuona hatufai, itoshe hiyo hiyo, dhamiria mwaka huu kuwa katu;
Sintojiambia ‘siwezi’
Sintojiambia ‘nitashindwa’
Sintojiambia ‘mi sipendwi’
Sintojiambia mi ‘sifai’

***Inaendelea ukurasa wa 9***



Makoleko Kalibonge

**“Mtaalamu yupi tena?” Badala ya kunijibu aliniuliza swali. Alinichanganya hata nikadhani nimekosea sehemu husika. Niligeukageuka mara kadhaa kuangalia mazingira ya pale. Nilijiridhisha kuwa sijakosea. Nilikuwa sehemu sahihi.**

“Mtaalamu huyu anayeishi hapa na ofisi yake ni hii hapa.” Nilijibu huku nikielekeza kwa kidole tena kwa uhakika wa nikifanyacho. Badala ya kunijibu yule kaka alisimama akanifuata nilipokuwa nimesimama. Kisha kwa upole sana aliniambia maneno ambayo yalinichanganya sana.

Sikuyaamini. Maneno ya yule kaka yalinimaliza nguvu. Nilihisi mwisho wangu umefika. Kila nililolifanya gizani lilikaribia kuanikwa hadharani. Watu watashuhudia.

“Pole sana dada,” aliniambia yule kaka baada ya kuniona nimefadhaika na habari zile. Sikutaka hata kuitikia wala kukataa. Niligeuza kurudi kituo cha daladala. Nilipanda daladala kurudi nyumbani.

Nilipoingia getini nilikutana na dada amekaa barazani akicheza na mwanawe. Aliponiona alianza kicheko kikubwa. Kisha dakika chache baadaye alianza kulia. Kilio hicho kilionesha huruma juu yangu na huzuni kwake. Aliniangalia kwa huruma. Bila shaka alitamani kuniambia kitu lakini alishindwa. Hivyo, aliendelea kulia.

Nami nilijikuta nalia bila kujua nililia nini hasa. Nililia kwa kumuona dada akilia kwa huruma namna ile au kitu gani? Nilipojikuta nazidi kulia, nilikimbia haraka kuingia sebuleni. Nilijitupa kwenye sofa. Nilinyamaza kulia lakini nikiendelea kukisikia kilio cha dada hapo nje.  Baada ya muda nilitulia. Niliyakumbuka maneno ya yule kaka kule Bagamoyo. Alisema, “Dada yangu, watu uwaonao hapo wamekuja kwenye arobaini ya huyo mtaalamu ambaye unamuulizia. Amefariki baada ya kuugua ghafla. Ukitaka kuhakikisha tuzunguke nyuma huko utaliona kaburi lake.”

***   *   ***

Muda umekwenda sana ndugu yangu. Tangu umefika sijakupa chochote – hata maji ya kunywa sijakupa. Hatujapishana sana kuingia humu ndani. Hazijafika hata dakika kumi tangu niingie humu na wewe ukaingia. Kama nilivyokuambia kuwa nimetokea Bagamoyo kuangalia namna gani naweza kusaidiwa ingawa jitihada hazishindi kudura.

Sasa utajua wewe namna ya kunisaidia; ikiwa utamueleza kwanza mume wangu, au utakwenda kwa mama na baba, au utakwenda gazetini au popote au utanipa ushauri na mawazo ya kuyafuata. Utaamua mwenyewe.

Lakini usinishauri kwenda kwa mganga mwingine. Sitaki kusikia hayo mambo tena.

**MWISHO**

**Ngurumo ya Mwandishi tunamshukuru sana Mwandishi Makoleko Kalibonge kwa hadithi hii tamu. Ni matumaini yetu kuwa umeburudika na kujifunza.**




**SAIKOLOJIA—WAZA MAWAZO CHANYA**

**Inatoka ukurasa wa 7**

Badala yake, tujitamkie mambo mazuri mazuri tu. kwamba;
'Hakuna kama mimi'
'Mimi naweza kufanya makubwa'
'Mimi napendwa na kila mtu'
'Mimi sintoshindwa'
'Mimi mzuri'
'Kwangu watakuja tuu'

Ipo nguvu ya kujitamkia mazuri, na kujiwazia mazuri, maana mazuri huja kwa mambo mazuri tu.
Asante saana,tena sana kwa kuwa nami,uniwie radhi pia, kutokana na sababu zilizokua nje ya uwezo wangu, mwezi February nilishindwa kuweka mada mpya, ikabidi kurudia mada moja wapo iliyopita. Bado naendelea kuweka ratiba vizuri ili ikiwezekana tusikose makala mpya kila mwezi. Maswali yalikua mengi kwa baadhi ya wafuatiliaji wa makala hii ya Saikolojia, basi tuendelee kwenda eehh, na tuzidi kuombeana pia.

Kwa mawasiliano nipate kupitia no. +255 763 013 206.
Madame Neema Mbilinyi Mgao.
Dodoma.
Tanzania.

*"Kusoma ni kuzaliwa upya"*

*Richard Mwambe*





Muamar Muhammad Abu Minyar Al - Gadafi

## Coup d'état: 1969 (Mapinduzi)

Serikali ya Idris ilizidi kutopendwa na watu katika miaka ya 1960; ilikuwa imezidisha migawanyiko ya kimapokeo ya kikanda na kikabila ya Libya kwa kuweka mfumo mkuu wa shirikisho la nchi hiyo kuchukua fursa ya utajiri wa mafuta nchini humo.

Ufisadi na mifumo iliyokita mizizi ya utetezi ilienea kote katika nyanja ya mafuta. Utaifa wa Waarabu ulizidi kuwa maarufu, na maandamano yalipamba moto kufuatia kushindwa kwa Misri mwaka 1967 katika Vita vya Siku Sita na Israeli; Utawala wa Idris ulionekana kuwa ni wa kuunga mkono Israeli kutokana na ushirikiano wake na madola ya Magharibi. Machafuko dhidi ya Magharibi yalizuka huko Tripoli na Benghazi, huku wafanyakazi wa Libya wakifunga vituo vya mafuta kwa kushirikiana na Misri.

Kufikia 1969, Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) lilikuwa likitarajia makundi ya wanajeshi wa Libya kufanya mapinduzi. Ingawa madai yametolewa kwamba walijua kuhusu Vuguvugu la Maafisa huru la Gaddafi, tangu wakati huo wamedai kutojua, wakisema kwamba walikuwa wakifuatilia kikundi cha mapinduzi cha Abdul Aziz Shalhi cha Black Boots. Shalhi, ambaye alihudumu kama mkuu wa wafanyikazi wa Idris, na kaka yake Omar walikuwa wana wa mshauri mkuu wa zamani wa Idris Ibrahim Shalhi, ambaye alikuwa ameuawa na mpwa wa Malkia Fatima mnamo mwaka wa 1954. Baada ya kuuawa kwa baba yao, wakawa vipenzi vya Idris.

Katikati ya 1969, Idris alisafiri nje ya nchi kwa mapumziko ya majira ya joto nchini Uturuki na Ugiriki huku kukiwa na uvumi ulioenea wa kutekwa nyara au mapinduzi yaliyoungwa mkono na Uingereza na ndugu wa Shalhi mnamo tarehe 5 Septemba. Maafisa Huru wa Gaddafi, wakitambua hii kama nafasi yao ya mwisho ya kuwazuia Washelhi kupindua utawala wa kifalme, na kuanzisha "Operesheni Jerusalem". Kama Maafisa Huru wa Gaddafi wasingewatangulia akina Shelhi, bila shaka wangeshindwa na vikosi vilivyounganishwa vya Abdul Aziz Shelhi, naibu kamanda wa jeshi la Libya, na familia mashuhuri huko Cyrenaica ambazo ziliunga mkono familia ya Shelhi.

Tarehe 1 Septemba, Maafisa Huru wa Gaddafi waliteka viwanja vya ndege, ghala za polisi, vituo vya redio, na ofisi za serikali huko Tripoli na Benghazi. Gaddafi alichukua udhibiti wa kambi ya Berka mjini Benghazi, huku Umar Muhayshi akiikalia kambi ya Tripoli na Jalloud akakamata betri za kukabili ndege za jiji hilo. Khweldi Hameidi alichukua hatamu ya kituo cha redio cha Tripoli na akatumwa kumkamata mwana mfalme Sayyid Hasan ar-Rida al-Mahdi as-Sanussi na kumlazimisha kuachilia madai yake ya kiti cha enzi. Hawakupata upinzani mkali na walifanya vurugu kidogo dhidi ya wafalme.

Mara baada ya Gaddafi kuondoa serikali ya kifalme, alitangaza msingi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Libya. Akiwahutubia umati kwa njia ya redio, alitangaza kukomesha utawala wa "msimamo na fisadi", "uvundo wake ambao umetuumiza na kututisha sote".

***Itaendelea...***

# SAKO KWA BAKO:

## PATRICK NKIKA: MWALIMU MWENYE ROHO YA VITABU

**Toleo hili limejikuta huko Mtwara. Mbele yetu tupo sako kwa bako na mwalimu kijana, Bwana Harusi wa zama hizi. Ni nani huyu?**



Naitwa patrick nkika
Nimezaliwa mkoa wa kigoma wilaya ya Kibondo. Ni mtoto wa kwanza kwenye familia ya watoto saba ya mr & mrs Nkika

Nimepata Elimu ya msingi shule ya msingi Kibondo, shule ya upili Gwegenyeza,sec school, baada ya hapo nikajiunga na compulink kenya computer Trining college na mwisho nikajiunga na Montessori kawekamo Teacher,s college. Kwa sasa ni Mwalimu katika shule ya msingi MUUNGANO iliyopo mkoa Mtwara wilaya ya Newala vijijini

Tabia yangu ya usomaji wa vitabu ilianza wakati nipo katika shule ya upili ambao nilibahatika kupata vitabu vichache vya hadithi vya mwandishi nguli wa stori nchini Tanzania ndugu Ben. Mtobwa ambapo nilisoma vitabu vyake kama Roho ya paka salamu toka kuzima ,Tutarudi na roho zetu na Dar-es-salaam usiku.

kuanzia hapo ni kajenga shauku ya kusoma stori za kipelelezi za waadishi wengine. Kwa hiyo baada ya kumaliza shule ya upili nilianza kuwatafuta waandishi mbalimbali na kusoma hadithi zao na hapa naandika baadhi ya waandishi ambao nimewahi kusoma hadithi zao,

1. Ben R. Mtobwa
2. ERICK SHIGOGO
3. A.E. MSIBA
4. HUSSEIN TUWA
5. PATRICKI .CK (wajina huyu)
6. KEVINI MPONDA
7. BAHATI MWAMBA
8. JAPHET NYANGORO SUDI
10. EDGAR MBOGO
11. TARIQ H. HAJI
12. IAM FRANK
13. EUPHRASE KEZILA HABI
14. DAN BROWN.
15. RICHARD MWAMBE

Hao ni baadhi ya waandishi ninao wakumbuka na ambao kazi zao ninazo katika maktaba yangu mpaka sasa .pamoja na kusoma hadithi nyingi kutoka kwa waandishi mbalimbali mwandishi ambaye nimesoma hadithi zake nyingi ni RICHARD MWAMBE .Ambae nimesoma Hadithi zake zote mpaka sasa alizo kamilisha.

Vitabu vina msaada sana katika maisha yangu mpaka sasa kwani kupitia vitabu nina amini kuwa kila kitu kinawezekana kama ukiweka juhudi ,nia ,maalifa na sara mafanikio huja.

Nina penda vitabu vya Hadithi za kipelelezi sana kuliko vinginevyo japo husoma. Mwandishi anae nikosha sana ni RICHARD MWAMBE.

Maoni yangu kwa watanzania wote waishio ndani na ya nchi tuipende lugha yetu ya kiswahili, Tupende kusoma vitabu na makala za kiswahili.
Tuwaunge mkono waandishi wetu wa Hadithi na vitabu mbalimbali wanaotumia lugha ya Kiswahili kwa kununua na kusoma kazi zao.

Mwisho Namshukuru sana MUNGU kwa yote anayemtendea mpaka sasa pia nashukuru jarida la Ngurumo ya Mwandishi chini ya mwandishi RICHARD MWAMBE kwa kuiona nafasi yangu kwake .

Asante sana

# SHAJARA YA MUUAJI—1

Na. Richard Mwambe



**2012, August 8**
**12:51 asubuhi**

**MIBINGIRIKO GUEST HOUSE**

MWILI wa mwanamke aliyekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka hamsini na hamsini na tano hivi ulikuwa umelala sakafuni kimya. Macho yaliyokodoa yaliufanya uonekane kama bado una uhai. Lakini haikuwa hivyo! Aziza Botole alikuwa marehemu. Upande wa kushoto wa kifua chake palipambwa na doa kubwa jekundu. Ilikuwa damu nzito iliyoganda tayari. Marehemu Aziza alikuwa sakafuni, chali, akiwa na nguo za ndani tu, juu na chini.

Kile chumba hakikuwa na mtu mwingine zaidi ya askari wa jeshi la polisi na meneja wa nyumba hiyo ya wageni, waliokuja kwa uchunguzi wa tukio hilo. Ilikuwa hali ya kuogofya sana. Kitanda kilikuwa kimetandikwa vizuri, mkoba wa ngozi alioutumia Aziza ulitulia kwenye meza ndogo iliyokuwa hapo jirani. Nguo zake zilikuwa juu ya kiti kilichokuwa upande wa pili wa chumba hicho. Haikuwa na haja ya ubishani, ilieleweka kuwa Aziza ameuawa.

Ni katika Jiji la Dar es salaam, Wilaya ya Temeke… Tandika na viunga vyake, ilijaa taharuki. Kila kona unayopita hadithi ni kifo cha Aziza. Si kwamba wanamjua! Hapana! Ila tu kwa sababu tukio limetokea katika kitongoji chao, basi hawakuwa na budi kuweka mikusanyiko japo ya wachache wachache ili tu kupeana umbea!

Nje tu ya nyumba hiyo ya wageni iliyojulikana kwa jina Mibingiriko Guest House, gari moja la polisi liliegeshwa. Wakazi waliofanikiwa kufika hapo waliwekwa mbali kidogo ili kupisha Jamhuri ifanye kazi yake. Simanzi! Kila kitu cha kichunguzi kilipokamilika, mwili wa Aziza ulifunikwa na kuwekwa kwenye machela tayari kuondolewa.

Aziza, alikuwa mwanamke wa haja, ijapokuwa hakuwa na uhai lakini umbo lake la Kimanyema lilinyanyasa hisia za vijana wale wa jeshi la polisi. Kiu! Mwili ulipakiwa garini na kuondolewa kupelekwa hospitali ya Temeke kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu.
Mara baada ya kufikishwa hospitaini katika chumba cha uchunguzi, askari kijana aliyekabidhiwa jukumu la kukusanya taarifa za mauaji hayo alikuwa kando akitazama jinsi daktari alivyokuwa akiifanya kazi yake. Pamoja naye alikuwapo ndugu wa marehemu akifuatilia uchunguzi huo. Mwili wa Aziza uliolazwa juu ya kitanda cha uchunguzi haukuwa na mikwaruzo wala michubuko. Ni jeraha moja tu la kitu chenye ncha kali, chenye umbo la pembe tatu. Kisu! Kisu cha namna gani? Chenye umbo la nyota.

"Muuaji ametumia kitu chenye ncha kali, ila siyo kisu..." Yule daktari mtu mzima akamwambia yule askari, Sajini Damasi Kamukwaya. Damasi akabaki akitazama titi la marehemu lililotobolewa vibaya. "Na kitu hicho kimezama mpaka kuufikia moyo ndiyo maana imempelekea mwanamke huyu kufa haraka," yule daktari akamalizia.
"Naweza kusema muuaji alikusudia, maana kitu hicho kuchoma titi, kuzama kifuani mpaka moyoni ni pigo linalohitaji nguvu..." Damasi akaongezea.

"Naam! Na katika kipimo changu hapa, hiki kitu alichotumia kimezama kwa sentimeta kumi kama si kumi na moja," daktari akaeleza. Mtaalam wa alama za vidole kwenye miili ya marehemu naye akathibitisha kupata alama za vidole kwenye ule mwili pamoja na kitasa cha mlango. Aziza alikufa na uzuri wake, kitandani pale alilala kama anayemsubiri mumewe ili waburudike. Alikuwa mrembo, mrembo wa asili. Yule daktari akaufunika ule mwili,"Msiuangalie sana msije mkautamani" akawaambia na kumwita mhudumu wa chumba cha maiti kuuchukua kuuhifadhi.

"Mtu utamtamanije marehemu?" Damasi akauliza. Yule daktari aliyekuwa akivua glavu zake akaacha zoezi hilo na kumtazama askari huyo kisha akasikitika.
"Kijana, ya huku tuachie wenyewe! We unafikiri huyo marehemu na uzuri huo na shepu hilo atalala mochwari salama? Watumishi wa vyumba vya maiti wengi washarukwa na akili, kuna mmoja tumemfukuza kazi, alikuwa anawashghulikia kabla hawajaingia kwenye jokofu..."
"Ushetani" Damas akamalizia na kuondoka zake kurudi kituoni tayari kuanza kukusanya tafutishi zake.

Asubuhi ya siku hiyo ilianza namna

hiyo, waenyeji walisema 'nuksi'.

Mbingiriko Guest House ilikuwa nyumba kongwe ya kulala wageni katika eneo hilo la Tandika. Kama ungekuwa mwenyeji basi unashuka kituo cha basi cha Mango halafu unachukua barabara iendayo kushoto. Siyo mbali, ni kama mwendo wa dakika tano tu. Ilisifika sana kwa matukio ya mafumanizi kwani wanawake wengi, wake za watu hufichwa humo na waume za watu hujificha hapo. Mara kadhaa ilifungwa kwa amri ya serikali ya mtaa huo lakini mmiliki wake Bwana Erick Ulomi alijua kuitumia pesa yake. Maneno mawili matatu, bia mbili tatu na viongozi wa mtaa, Siku inayofuata kibao cha 'NAFASI ZIPO' Kingening'inia mlangoni mwa nyumba hiyo.

Utulivu ulirejea, lakini watu wote waliolala hapo walizuiwa kutoka, walitakiwa kusubiri mahojiano maalumu na afisa wa polisi kutoka Kituo cha Chang'ombe.

❦ ❦ ❦

Habari ya mauaji ya Aziza ilififia ndani ya siku mbili tu, kila mtu aliendelea na shughuli zake. Watu wote waliokuwa ndani ya ile nyumba walihifadhiwa kituoni. Baada ya mahojiano ya siku tatu ndipo polisi walipoona kuwa kati yao hakuna muuaji. Kwani kila mmoja alikiri kuwa hakuna kelele iliyosikika tofauti na zile za kimahaba tu. Wote waliachiwa huru, wengine walikuwa wake za watu na wengine waume za watu. Songombingo!

Kifo cha Aziza kilivunja ndoa kadhaa kwenye jiji la Dar es salaam kwa kuwa baadhi ya waume, wake zao walihifadhiwa polisi siku tatu na wake nao vivyo hivyo. Vichwa viliwauma, lakini kazi yao waliijua. Mara baada ya kumalizana na *'wageni wenyeji',* wapelelezi wa kituo hicho cha Chang'ombe walianza mahojiano na wafanyakazi.

"Aziza aliingia alilala pale gesti tangu Jana yake!" Akaeleza mmoja wa wasichana wanaofanya kazi katika gesti hiyo.
"Aliingia na nani?" Yule askari akauliza.

**Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865**

"Kila anapokuja huja peke yake halafu baadae huja mwanaume anayetaka kuwa naye,"
"Mwanaume gani alikuja usiku wa siku hiyo?"
"Aziza hakuwa na mwanaume mmoja. Usiku wa Jana alikuja mbaba hivi, ana mandevu mengi, mrefu, mweusi..."
"Unakumbuka alivaaje na alikaa kwa muda gani?"
"Alivaa shati la kahawia na suruali nyeusi... Alikuwa pale kama masaa manne hivi... Aliondoka usiku sana..."

Wale askari wakatazamana, hisia zao zikawatuma kuwa huyo ndiye muuaji.

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Yule aliyekuwa akihoji maswali akarudisha macho kwa Ujoro. Ujoro Mohammed alikuwa mhudumu katika nyumba hiyo ya kulala wageni ya Mibingiriko. Ijapokuwa wengi aliyowapangisha hawakuwa wageni, ye hakujali. Cha muhimu pesa iliingia. Na bosi wake Bwana Ulomi alikuwa akimkubali sana Ujoro. Alimwamini, akaaminika.

Alikuwa mtunza siri aliyekula yamini. Wengi walioingia hapo aliwajua kwa sura, majina hata hali zao za ndoa. Kwakuwa walikuwa wakimtoa kwa pesa za soda, alificha siri.
"Huwa mna utaratibu gani kama mtu anaondoka huku mwenzake kamwacha chumbani?" Hilo lilikuwa swali gumu kidogo lililohitaji tafakari ya wastani.

"Hakuna!" Ujoro akajibu.
"Kwahiyo tukisema huyo bwana ndiye muuaji utakubali?" Akaulizwa.
"Hapana!"
"Kwanini?"
"Kwa sababu usiku huo mara baada ya yule mwanaume kuondoka, alfajiri kama saa kumi hivi alikuja mgeni wake mwingine kijana kijana hivi..."
"Ina maana alilala na wanaume wawili kwa usiku mmoja?"
"Hah wawili tu! Wakati mwingine hata watatu..." Ujoro akazidi kufunguka. ***Itaendelea...***

**Ilipoishia…**

**Akaichukua ile bahasha na kuiondoa lakiri iliyowekwa kwenye mfuniko wake. Ndani ya bahasha ile kulikuwa na karatasi kadhaa zilizochapwa kwa mashine. Akazivuta nje. Zilikuwa zimefungwa vizuri na kubanwa kama kitini safi.**

***Endelea...***

Kwa mara ya kwanza alihisi mikono yake ikimtetemeka kama mgonjwa wa kiharusi. Kilikuwa kitini chenye karatasi nne, nzuri, zenye manukato. Juu yake kulikuwa na maandishi makubwa tu yaliyosomeka, CRONOC 7. Maandishi yale yaliyokutana na macho ya Amata yaliufanya moyo wake kwenda mbio kuliko kawaida. Alihisi baridi likipita kwenye mishipa ya damu kuelekea miguuni. Moyo wake ukamzuia kufungua kurasa ya pili.

Lakini nilizichukua za nini? Akajiuliza kisha akafungua kurasa hiyo. kurasa ilieleza juu Cronoc 7 kuwa ni kitu gani. Lakini maelezo hayo hayakuweza kuleta maana ya moja kwa moja. Amata alijikuta akikodoa macho, asielewe. Akarudisha zile karatasi ndani ya ile bahasha na kuwasha gari lake. Akatoka eneo lile na moja kwa moja akaelekea nyumbani kwake Kinondoni.

**SURA YA 06**

KUSINI MASHARIKI mwa Nigeria ndiko linakopatikana jimbo la Anambra. Jina lake la Anambra lilitokana na lile la 'Oma Mbala'. Nchi hiyo inayosifika kwa utajiri wa mafuta, taifa lililopo Afrika ya Maghalibi ndipo alipotakiwa kufika Mr. Codec au mwite 'Code C'.

Majira ya jioni ya siku hiyo ndege iliyomsafirisha kiumbe huyo ilikanyaga ardhi ya jimbo hilo, katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Akanu Ibiam. Saa moja baadae Codec alikuwa akitoka taratibu, tayari akiliacha lile jengo la uwanja huo na kuelekea kwenye maegesho ya taksi.

Mbele yake kama hatua ishirini hivi alisimama mtu mmoja wa makamo, sio mzee sana wala si kijana, mkononi mwake alikuwa kakamata kitu kama kasha hivi. Hiyo ilikuwa ni isahara tosha kwa Codec kujua kuwa huyo huenda akawa ni mwenyewji wake. Lakini hata hivyo alisubiri jambo lingine la utambulisho.

"Mzee! Mzee!" yule mtu akaita, "karibu Anambra, unahitaji panya wa kununua ama wa kula?" yule mtu akauliza.

Codec akasimama na kumtazama mtu huyo juu hadi chini, "kama umeona kuwa paka ndiyo kiumbe wa kula panya basi nataka". Alipomaliza tu kusema hayo yule mtu akanyakuwa mizigo ya Codec na kuipakia kwenye Ford Everest iliyokuwa jirani na hapo aliposimama.

"Karibu sana Anambra, mji wa kupendeza wenye watu wa kila aina, matajiri kwa masikini, wazuri kwa wabaya, weupe kwa weusi na hata warembo wa aina zote utakazo…"

"Asante sana,"


"By the way naitwa Azu Omil," akajitambulisha.

"Naitwa Codec au niite Code C," akajibu mgeni huyo.

"Oh! Nafurahi kukufahamu, hoteli gani unapenda kufikia?" akamtupia swali lingine.

"Benizia Hotel tafadhali…"

"Waoh! Onitsha hiyo, umeipata comrade… tena pale pana warembo wa Kinaija, sampuli zote utakazo; warefu wembamba, wanene wafupi, wenye makalio makubwa kwa madogo, wenye viuno vya nyigu na wale wenye miili kama sanamu za michelini, bila kusahau wenye shepu ya mswaki, watakukandakanda ili kesho uamke fresh," Azu akamwambia Codec.




"Hahahahaaaaaa! Nimesahau hata ladha ya mwanamke, sijui hata wanafananaje kwa sasa," Codec akacheka na kueleza.

"Sasa wewe una starehe gani?"

"Sina starehe,"

"Haiwezekani!"

"Inawezekana, starehe yangu ni kutokuwa na starehe. Sikia Azu epuka sana starehe na wanawake hasa unapokuwa na mambo mazito na magumu ya kuamua na kutenda. Maana mwanamke huisimamisha akili yako na kukubakishia utashi tu," Codec akaeleza na Azu akabaki kimya akiendelea kupanga na kupangua gia za lile Ford.

Baada ya ukimya wa dakika kama saba hivi, Azu aliegesha gari kwenye hoteli moja ya kawaida tu. Kibao

cha Benizia kilimlaki Codec au Code C kama alivyopenda kujiita.

"See you!" akamuaga yule mwenyeji wake kisha yeye na mkoba wake mdogo na begi lingine mkononi akavuta hatua na kuingia katika hoteli hiyo. Azu akaondoa gari bila kuchelewa kwani kazi yake ilikwisha kwa siku hiyo.

Baada ya kukamilisha taratibu za hapo, alipelekwa ghorofa ya nne. Akaingia katika chumba kikubwa chenye kitanda kimoja cha tano kwa sita, na sofa la mtu mmoja lililotulia kwenye kona likiwa na meza ndogo ya kioo na jokofu la wastani. Akatupia ule mkoba wake kitandani naye akaingia maliwato kujiswafi.

Alipoingia huko, moja kwa moja alisimama mbele ya kioo kikubwa kilichotundikwa ukutani. Alipotaka kufungua bomba kwa ajili ya kunawa mikono, simu yake ikaita. Akaichomoa mfukoni na kuitazama. Hakuipokea. Alindelea na shughuli yake. Na alipomaliza akatoka tena chumbani na kujiweka juu ya kitanda.

*Didiof Mathis, Anambra 650!* akawaza kibarua kilichokuwa kikimsubiri mbele yake. Ile simu ikaita tena. Akainyakua na kuiweka sikioni.

"…You have 48 hours to leave Nigeria, just kill him…"

Aliambiwa ana saa arobaini na nane tu za kuwepo Nigeria. Aliikata ile simu na kuitupa kitandani kisha ukimya ukambeba.

⚜

Maisha katika mji wa Anambra yalikuwa yaleyale ya Kiafrika. Hakukuwa na tofauti na maisha ya Mombasa au Tanga. Kila mtaa na barabara zilijaa watu na biashara ndogo ndogo zilizokuwa zikiendelea hapa na pale. Walevi walionekana wakiyumbayumba barabarani alikadhalika makahaba nao walikuwa wakijivinjari kwenye baadhi ya vichochoro na barabara zinazopitwa na vibopa. Lengo lilikuwa ni kuwanasa wakiwa ama wanatoka katika starehe au wanaenda. Na hakika walipata wengi kwani wapo waliojipitisha makusudi ili kujipatia 'tamtam' hiyo.

Codec akiwa kwa mwendo wa miguu jioni hiyo ambapo bado giza lilikuwa halijachanganya sana, alijionea haya yote yakiendelea. Afrika! Akajisemea moyoni huku akiona watoto wakikimbizana barabarani pasi na kuogopa magari yanayopita eneo hilo.

Katika pitapita zake, baa moja ilimvutia. Baa ya kisasa iliyokuwa ikipigwa muziki wa Jazz ambao ulisikika vyema kupitia spika nzuri zilizofungwa katika kona zake. Akasimama na kutazama upande ule. Kisha akakata shauri na kupotelea ndani. Kwake hakujiona kama mgeni kwa kuwa ndani yake alikutana na 'weupe' wengi tu na wala watu hawakumshangaa kwa kuwa naye alionekana ni 'walewale' tu.

"Welcome! This way please…" sauti ya mwanamke ilimgutusha na kumtaka kufuata uelekeo anaooneshwa. Hilo lilitokea wakati Codec alipokuwa akishangaashangaa wapi aketi. Hakuuliza wala kuhoji akamfuata mwanamke huyo ambaye alitangulia mbele na mkononi mwake alikuwa na chano tupu. Katika moja ya meza nyingi zilizokuwa katika baa hiyo, aliketi pembeni karibu na maua makubwa, akiendelea kuburudika na ule muziki wa Richard Bona. Baada ya kuletewa kinywaji na kuwekwa mezani na mwanadada yule yule, alimkamata mkono. Yule mwanamke akamtazama Codec kwa jicho pembe.

"Unaweza kuketi nami hapa?" akamwuliza.

"Kwa sasa ni ngumu maana nina wateja wengi labda baadae kama utakuwepo," yule mwanadada akajibu.

"Ok, je, wataka kuipoteza nafasi hii adimu?" akamtupia swali lingine.

"Kivipi?"

"Kwa kuniitia mwanamke mwingine anayenifaa,"

Yule mhudumu hakujibu, aliendelea kumtazama mzungu huyo huku akili yake ikipingana na moyo wake. Lipi la kuamua!

"Subiri kidogo, nakuja," akajibu yule mhudumu kwa kiingereza chao cha ki-pidgin.

"Siku zote mwanamke atakupa siri uitakayo cha muhimu ni kumkoleza kwa kinywaji na kumtia pesa iliyotakata. Codec nina shida gani na pesa? Zipo. Ninazo. Ndiyo, huyuhuyu lazima nimtumie katika hili, akija kurudiwa na fahamu saa 48 zimepita mwanaume nabadilisha kiwanja…" ***…Itaendelea***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani muda wowote kutoka sasa.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

***Inaendelea…***

Muuza duka akachukua chupa ndogo iliyokuwa na vidonge vyeupe kisha akampatia Marjane. " hizi zitampa nafuu, mpe vidonge viwili kila baada ya saa mbili."

"Ahsante sana!" alisema Marjane. Kisha akaenda nyumbani na kusubiri.

Kesho yake asubuhi, alirudi kwa muuza dawa tena. Kwa mara nyingine tena akaongea kwa nguvu ili kila aliye pale dukani asikie anachokisema.

"Bosi wangu Kassim hajapata nafuu hata kidogo!" alisema Marjane kumwambia muuza dawa. "badala yake sasa hali inazidi kuwa mbaya, unaweza kunipatia dawa nyingine ili aweze kupata nafuu?"

Muuza dawa alitikisa kichwa kwa kusikitikia hali ya Kassim. "Pole sana, kwa kusikia hali ya Kassim kuwa mbaya kiasi hicho" alisema huku akichukua chupa ya dawa na kumpa Marjane. "Mpe hii anywe vijiko viwili itamfanya apate usingizi na maumivu yatapungua."

"Ahsante sana" alijibu Marjane na kuondoka kwenda nyumbani.

Jioni ya siku inayofuata, jua lilipokuwa linazama, baadhi ya watu walikuwa wakipita katika nyumba ya Kassim, wakasikia kilio kikali sana. Alikuwa ni mke wa Kassim.

"Kassim amefarikiii!!!" alilia mke wa Kassim. "Masikini mume wanguuuu!! Umefarikiii!! Nitafanya nini mimiiiii!!!

Marjane akaenda kwa fundi wa nguo aitwaye Mustafa. "Mustafa!" Marjane alisema huku akimuwekea sarafu ya dhahabu mkononi kwake.
"Nimesikia watu wakisema kuwa wewe ni fundi nguo mzuri sana hapa mjini. Nina kazi ngumu sana nataka kukupa. Kumetokea ajali na kuna mtu amefariki kwa ajali hiyo, hivyo basi, nataka umtengenezee suti nzuuuri sana ili tuweze kumzika vizuri. Tutakulipa vizuri sana ila usimwambie mtu yeyote kuhusu hili. Mtu huyo ameuliwa kwa kukatwa na mapanga hivyo hakikisha hakuna mtu atakayeweza kuona alama yeyote ile."

Mustafa akaangalia ile dhahabu aliyowekewa mkononi. "Nitaifanya usiwe na wasiwasi" alisema. "Lakini nitahitaji dhahabu nyingine zaidi ili



niweze kuifanya hii kuwa ni siri."

"Utapata zaidi dhahabu, usijali" alijibu Marjane. "Lakini lazima uifanye kuwa ni siri. Sitakwambia kuwa mtu mwenyewe ni nani na anaishi wapi. Nitakapokupeleka kwake lazima uvae kitambaa machoni ili usiweze kujua ni wapi."

"Vizuri sana!" alijibu Mustafa fundi nguo. "Nitafanya kama ulivyosema."

"Sawa basi, chukua sindano yako na uzi" Marjane alimwambia. "kisha twende huko pamoja sasa."

Marjane akachukua kilemba change na kumfunga fundi vizuri machoni kuzunguka kichwa chake. "Unaweza kuona chochote?" alimuuliza.

"Sioni chochote" fundi alimjibu.

"Vizuri!! Sasa twende nyumbani sasa hivi" alimwambia.

Marjane alimuongoza Mustafa mpaka nyumbani kwa Kassim na kumpeleka hadi kwenye ghala ambapo ulihifadhiwa mwili wa Kassim. Kisha akamfungua kile kitambaa machoni na kuuona ule mwili.

"Unataka nimtengenezee huyu suti!!? Ni kazi ngumu sana." Alisema Mustafa. "Nahitaji dhahabu nyingine zaidi!"

"Utapata," alijibu Marjane na kuweka sarafu mbili nyingine za dhahabu kwenye mkono wa Mustafa. "Lakini unatakiwa uanze kushona sasa hivi kwasababu tunataka kumzika huyu usiku huu huu."
Mustafa akachukua sindano na uzi wake na kuanza kushona.

Mustafa alishona kwa muda mrefu sana huku Marjane akimsubiri kwa wasiwasi. Mustafa alipomaliza kushona suti nzuri ya hariri alifungasha vifaa vyake kisha Marjane akamfunga tena machoni kile kitambaa na kumuongoza tena kurudi hadi nyumbani kwake.
Walipofika, Marjane akamfungua kile kitambaa na kukiweka begani kwake. "Sasa unaweza kuendelea na kazi zako zingine." Alisema Marjane kumwambia Fundi Mustafa, "sahau kila kilichotokea siku ya leo."

***Itaendelea toleo lijalo***

**Kutoka Instagram.**
Machi 23, 2024 Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alikutana na kamati iliyoundwa na Wizara kuendesha Tuzo ya Uandishi Bunifu na Uongozi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kujadili maandalizi ya Tuzo ya mwaka 2024.

Akizungumza na vyombo vya habari baada ya kikao Prof. Mkenda amesema Tuzo hiyo inachochea uandishi nchini kwani tangu ianzishwe mwaka 2023 kumekuwa na mwamko mkubwa wa maandiko mengi kutoka kwa waandishi hapa nchini.

Amewataka Watanzania kuongeza ari ya usomaji na kuendeleza utamaduni wa kuandika

Mwenyekiti wa kamati ya Tuzo, Prof. Penina Mlama, amesema miswada zaidi ya 200 imepokelewa kutoka kwa Watanzania.

“Tumeendelea na maandalizi hasa kwa upande wa kuchambua miswada iliyowasilishwa, kwa sasa majaji wanasoma miswada yote na ndiyo wataamua washindi ni kina nani” amesema Prof. Mlama.

Aidha Murugenzi Mkuu wa TET , Dkt. Aneth Komba ameeleza kuwa Tuzo hii ni alama tosha ya kuonesha uwezo shindani uliopo kwa waandishi bunifu nchini.
Ametaja Nyanja tatu zinazoshindaniwa kuwa ni

## ABDULRAZAK GURNAH KUWA MGENI RASMI

vitabu.

“Tuzo hii ni hamasa kubwa ya uandishi hapa nchini kwani tangu ianzishwe imechochea waandishi wengine kuweza kuwasilisha maandiko mbalimbali ambayo mengi yanaonekana kuwa na maudhui bora yatakayoongeza wigo wa vitabu vya kusoma hususan katika shule, vyuo na jamii kupitia Maktaba” amesema Prof. Mkenda

Prof. Mkenda ameongeza kuwa uandishi bunifu ni sehemu ya kukuza na kuhifadhi lugha na utamaduni wa Mtanzania ambayo imehimizwa katika Toleo la 2023 la Sera ya Elimu na Mafunzo na Mitaala mipya.

Amebainisha kuwa mwaka huu kilele na utoaji Tuzo itakuwa tarehe 13 Aprili, 2024 jijini Dar es salaam na Mgeni Rasmi ni Mshindi wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi 2021 Prof. Abdulrazak Gurnah.

riwaya, ushairi na hadithi za watoto.



**Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.**

# SHUBAKA LA VITABU

**Katika safu yetu ya Shubaka la Vitabu, toleo hili linaangazia Maktaba 10 bora katika Afrika. Kupitia safu hii utajifunza na utajuzwa mengi kuhusiana na vitabu, maktaba na mengine mengi. Endelea kuwa nasi.**

## 1. MAKTABA YA ALEXANDRIA—MISRI

Maktaba maarufu zaidi barani Afrika ni Maktaba ya Alexandria - ni jina la heshima la sasa kwa maktaba maarufu ya zamani.
Maktaba hii ipo kwenye ufuo wa Alexandria karibu na mahali maktaba ya zamani ilikuwapo. Maktaba inatoa nafasi ya kutosha kwa zaidi ya vitabu milioni nane.
Gharama ya ujenzi wake wa ajabu imeacha maktaba kuwa na pesa kidogo za kununua vitabu. Ingawa kufikia sasa hivi, mkusanyiko huo ni karibu milioni moja. Nusu yake ilitolewa kutoka Maktaba ya Kitaifa ya Ufaransa.

Maktaba hiyo ina mkusanyo mkubwa zaidi wa vitabu vya lugha ya Kifaransa barani Afrika na ya sita ulimwenguni. Mengine mengi yameandikwa kwa Kiarabu na Kiingereza.

Jumba hili pia lina kituo cha mikutano, makumbusho manne, majumba ya sanaa kumi na tisa, uwanja wa sayari, maabara ya kurejesha hati, maktaba ya media titika, maktaba ya ramani, maktaba maalum ya wasioona na nakala pekee duniani.



Jengo la kizamani la Maktaba ya Alexandria huko Misri

## 2. MAKTABA YA MONASTERI YA MT. CATHECRINE

Monasteri ya Mtakatifu Catherine ilianzishwa mnamo 381 na inachukuliwa kuwa monasteri kongwe zaidi ulimwenguni.

Maktaba yake ilijengwa wakati fulani katika karne ya sita, ambayo inafanya kuwa maktaba ya zamani zaidi inayoendelea duniani mpaka sasa.

Kama unavyodhania, maktaba hii ina mkusanyiko wa ajabu, ikijivunia zaidi ya kodi 3,500 katika lugha mbalimbali - ya pili baada ya ile ya Vatikani. Nimojawapo ya milki muhimu zaidi ya monasteri ni Achtiname, ambayo ina ahadi kutoka kwa Muhammad mwenyewe inayotoa ulinzi wake kwa nyumba ya watawa.

Maktaba hiyo pia ilikuwa na Biblia ya zamani zaidi ambayo ilikuwa karibu kuhifadhiwa kabisa, lakini tangu wakati huo imesafirishwa hadi Urusi na kisha kuuzwa kwa Maktaba ya Uingereza.

Maktaba hii ipo katika shina la Mlima Sinai huko Misri.

Monasteri ya Mtk. Katarina—Sinai (Misri)



# KITABU NILICHOSOMA

## Richest Man Of Babylon

**MWANDISHI:** GEORGE S. CLASON
**MSOMAJI:** APLON CHAPUGA.
**KUTOKA:** KOROGWE TANGA.

Hii ni simulizi inayohusu himaya ya kale iliyoitwa Babylon . Historia inaonesha himaya hii ilikuwa ndani ya Iraq ya sasa.

Ndani ya Babylon kulikuwa na tajiri mkubwa aliyejulikana kwa jina la ARKAD.Siku moja rafiki zake wa ujanani walimfuata na kumuuliza maswali kuhusu mafanikio yake.

Swali kubwa walilomuuliza ni kwanini wamecheza wote,wamekua pamoja,wamesoma pamoja iweje yeye awe tajiri tena wa kupindukia na wao wamebaki maskini?

ARKAD akawajibu "mwalimu wetu alitufundisha kuwa ukiwa darasani unafundishwa mambo mawili, la kwanza ni mambo unayofundishwa na kuyaelewa papo hapo lakini jambo la pili ni lile ambalo unaambiwa ukatafute ufumbuzi ,hili la pili ndilo nililo lishika zaidi".

Aliwaambia kuwa ktk harakati zake za utafutaji siku moja alikutana na mkopeshaji ambaye pia alikuwa tajiri ndani ya Babylon.Baada ya kuchukua mkopo hakuweza kurejesha kwa wakati kitendo ambacho kilimpelekea kuwa mtumwa wa bwana huyo Kwa kufanyishwa kazi ngumu pamoja na kuchapwa viboko.

Hatimaye adhabu yake iliisha lakini kwa kuwa azima yake ilikuwa kupata utajiri alipokutana na bwana wake hakusita kumuuliza.Swali alilomuuliza ni je afanye nini ili awe tajiri?

Yule bwana tajiri alicheka sana,akamwambia ARKAD ili nikuambie kuna kazi nitakupa,Arkad akamjibu kuwa yupo tayari ilimradi tu aambiwe Siri ya utajiri ni nini.Alifanya kazi usiku kucha bila kulala.Asubuhi ikafika na yule bwana tajiri akajongea alipokuwa ARKAD.ARKAD akamwambia bwana wangu kazi uliyonipa nimemaliza na sasa nasubiri ahadi yangu!

Bwana yule aitwaye ALGAMISH akamwambia mwanangu,wewe huwalipi wanaokuuzia viatu? Huwalipi wanaokuuzia mavazi? Huwalipi wanaokuuzia chakula? Hutumii pesa Kwa matumizi ya kila siku hapa Babylon? Je,unabakiwa na nini? ARKAD akamjibu sibakiwi na chochote!

ALGAMISH akamwambia *" if you did keep for yourself one tenth of All you earn, how much would you have in ten years?" Akaongezea na kusema "Wealth, like a tree ,grows from a tiny seed.The first copper you save is the seed from which your tree of wealth shall grow.The sooner you plant that seed the sooner shall the tree grow."*


ARKAD akawaambia rafiki zake kuwa baada ya kuambiwa maneno hayo akaamua kuchukua hatua kwa kujiwekea akiba na akiba hiyo kuifanyia biashara .Mwishowe mzee ALGAMISH baada ya kuona uwezo wa ARKAD akamfanya kuwa mbia ktika biashara jambo ambalo lilimkuza zaidi na zaidi na kuwa tajiri mkubwa sana katika himaya ya BABYLON.

Marafiki zake wakumuuliza sasa wafanye nini ili na wao wawe na mali ?

ARKAD akawashauri watembee na maneno haya *"A PART OF ALL I EARN IS MINE TO KEEP"*

Maneno haya wayaseme wanapoamka ,mchana ,jioni na wanapolala hakika watafanikiwa.
Rafiki zake waliondoka kwa furaha huku wakiahidi mabadiliko.

AHSANTE SANA NAOMBA KUWASILISHA.






TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Usilie wala usicheke
Usibeze wala wala usigadhibike
Usinune wala usihangaike
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Maisha kigeugeu
Ukicheza ‘tapata ngeu
Magumu ka’ mwamba geu
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Gotika
Sujudika
Allah mmoja hakika
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Shamba lima
Uza umma
Kula kwa uma
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Tupu uza
Ishi Buza
Ni mauzauza
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Dada danga
Mzee wanga
Kijana tanga
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Gari lako
Nyumba yako
Shida zako
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Kilio chako
Nung’uno lako
Ujinga wako
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Wengine wanazo
Wengine hamnazo
Elimu si uwezo
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Njano kijani ni rangi
Nyekundu nyeupe ni rangi
Dodoma kuna wagogo na warangi
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Usimnunie nenene
Nenda na wewe kapambane
Wembamba siyo unene
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Yalivyo ni vivyo hivyo
Yaani yako hovyo hovyo
Mwenye nacho ni mchoyo
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Usimdharau mtu, huijui kesho yake
Dunia siyo ya mtu, Mungu ana muda wake
Usimwite kidudumtu, kesho utagonga kwake
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Bahatisha bahati
Hababahatishi mwenye bahati
Hutopata kwa bahati
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo

Yote kwa yote piga kazi one day utaibuka, hakuna aliyezaliwa na utajiri… ni ama ameukuta au kautafuta.

Maneno nimemaliza, ushujaa meonesha
Mengi yameshaniliza, mara nyingi nimekesha
Mungu si wako ajuza, Siku akanionesha
Maisha ndivyo yalivyo, yalivyo ni vivyo hivyo.

***Shujaa Maneno***
***Bagamoyo—Pwani***
***Machi 2024***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha

Wana-UWARIDI kwenye picha ya pamoja na mwandishi wa vitabu Willibard Makene katika uzinduzi wa vitabu vyake; UCHOCHORO WA TANZANITE na UFAFANUZI LUGALO







Prof. Penina Mlama akionesha moja ya kitabu kilichozinduliwa siku hiyo.




Katika picha ya pamoja, baadhi ya wageni waalikwa waliofika katika uzinduzi wa vitabu UCHOCHORO WA TANZANITE na UFAFANUZI LUGALO vilivyoandikwa na Willbard Makene (mwenye fulana nyeupe). Uzinduzi ulifanyika kwenye viwanja vya Elite Bookshop Mbezi.



Prof. Emmanuel Mbogo, mwandishi wa kitabu 'WATOTO WA MAMA NTILIE' naye alikuwapo kati ya wageni muhimu waalikowa.

**'VITUKO VYA UHURU' - Harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika na vituko vyake. Ni kitabu kilichoandikwa na M.W. Kanyama Chiume—1973. Hii ni Kutoka Maktaba**

**Huko pia tukakuta sherehe kubwa sana na huku watu kwa mamia wanaimba Watu wa TANU wafile.**

Kwao tulikuwa tumekufa maji mtoni, na hivyo Bwana Mfalimbenga, Mzagila na mshauri mkubwa wa Chifu Towagale alistuka sana kuona tumesimama mbele yake tukiomba msaada wake huku tukitetemeka kwa baridi tukiwa tumechoka, tuna njaa na tumelowa. Akituonea huruma, alitoa amri tukokewe moto na kupewa chakula."

"Nini madhumuni ya TANU?" aliwauliza ndugu Lila na mwenzake. "Tulichukua nafasi hiyo," alieleza ndugu Lila, "kumwondoa kasumba ya mkoloni."
"Bila uhuru," walisisitiza "machifu wataendelea kuwa viatu vya mkoloni."
"Sidhani kama chifu atawaruhusu kufanya mkutano ama kufuangua tawi la TANU: nina wasiwasi anaweza hata kuwafunga," aliwaambia.
Usiku ule ndugu Lila Mwinyikondo na mwenzake walilala juu ya vitanda vya majani katika kibanda kichafu sana ambako mbu walikuwa kana kwamba wanawangojea. Nguo zao walizikausha kwa moto ambao pia ulikuwa kama blanketi lao usiku ule.
Chifu alifoka sana alipowaona asubuhi yake wakimsihi awape ryhusa kufanya mkutano na akakataa kabisa kutoa kibali hicho. Walitiwa msukosuko miubwa sana na ikawabidi warejee Malinyi wakichukua njia ndefu kukwepa kuvuka mto tena kwa mtumbwi. Mara tu walipofika Malinyi, wakakamatwa na kuwekwa kizuizini kwa Mzagila wa Karim, Bwana Mpangachuma, kwa muda wa miezi miwaili.

Wananchi wengine zaidi walitiwa jela miongoni mwao akiwamo John Kawelewele, Antoni Mgawai, Omary Kwamba, Almasi Mkapila, Ali Kanguma na Francis Mbule. Donald Chiyao aliyekuwa amechukua shilingi 500.00 zilizokusanywa kwa siri Ifakara, kuwatetea waliokuwa jela, alikufa kifo kisichoelezeka. Pia Ahmed Kawamba, kaka wa Omary Kawamba, inasemekana aliburuzwa na wapinzani wa TANU alipokwenda kumsihi Mtemi Towagale kuwaruhusu wafungue tawi la TANU, na kuuawa.
"Lakini kufungwa kwetu," alieleza ndugu Lila, "kulitusaidia sana. Bwana Mpangachuma alitupa msaada mkubwa. Tuliweza kwenda hadi misheni ambako padre mmoja, kwa siri, alituagizia kadi kutoka Dar es salaam. Hali kadhalika, ingawa hatukuwa na ruhusa ya kukutana na watu, wengi walikuja kwa siri kukata kadi za TANU. Pia baada ya kutuma barua kwa siri kwenda Dar es salaam kuhusu kifungo chetu, Mwenyekiti wa Kamati Kuu Bwana Clement Mtamila na Steven Mhando, Katibu Mkuu wa TANU, walikuja Malinyi kututetea. Hawakufanikiwa na ikawabidi kulala sokoni kwenye mvua na baridi kwa kuwa watu waliogopa kuwakaribia.
"Hatimaye Mwalimu Nyerere alipoonana na PC na Gavana, tukaachiwa huru. Waliofungwa Kidatu pia wakatolewa baada ya mwezi mmoja kutokana na juhudi za Mzee Chamwenyewe na Idi Lubumba. TANU iliwawekea wakili kutoka Iringa. "Hata baada ya kuachiwa huru, Chifu mdogo Karimu alikataa kabisa kuturuhusu tufanye mkutano kwa vile hakutaka kile alichokiita Vita vya Maji Maji nchini mwake.

Wakoloni walimpumbaza Chifu Towagale kiasi kwamba alidiriki hata kumkataza Mwalimu Nyerere kufanya mkutano katika eneo lake. Lakini vuguvugu lilianzishwa na ule mkutano wa siri msituni Mahenge. Woga ulianza kuwatoka watu. Siasa ya TanU ilianza kuenezwa polepole pote wilayani. TANU ikawa na nguvu kubwa kiasi kwamba wakati wa sherehe za Saba Saba 1958, Chifu Towagale akiwa na ngao na mkuki mkononi na akicheza huku na huko, kwa unyonge aliuambia umma, 'Sikufanya makusudi kuikataa TANU. Kwa vile baba yangu Chifu Kiwanga, alikufa kutokana na vita vya Maji Maji niliogopa kwamba TANU ingeleta vita vya Maji Maji tena nchini.'"

***Umma ukiamua, hauwezi kuzuilika kufikia lengo lake.***

***ITAENDELEA...***

# ELIMU JAMII

## Ukamataji, Upekuzi na Dhamana ya Polisi—1

**MAANA YA UKAMATAJI**

Kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 1985, ya mwenendo wa makosa ya jinai iliyofanyiwa masahihisho mwaka 2002. Ukamataji ni kitendo cha **kumzuia** mtu au **kumnyima** mtu uhuru wake wa kwenda **anakotaka**, ili afikishwe kituo cha Polisi kwa ajili ya upelelezi na hatimaye afikishwe mahakamani kujibu shitaka linalomkabili.

***Ni wakati gani mtu atahesabiwa kuwa amezuiliwa?***

i) Mtu atakuwa amezuiliwa ikiwa atakuwa mikononi mwa afisa wa Polisi, kwa madhumuni yanayohusiana na upelelezi wa kosa la jinai na kwamba afisa Polisi hawezi kumwachia wakati wakati akiwa katika ulinzi wake halali kutokana na kosa analotuhumiwa kutenda na kulifanya.

ii) Mtu atahesabiwa kuwa amezuiliwa kihalali au kisheria, iwapo atakuwa ameongozana na afisa wa Polisi au atakuwa anayesafiri naye katika gari kwa madhumuni ya upelelezi.

**Ni wakati gani mtu atahesabiwa kuwa yuko chini ya ulinzi?**

Mtu atahesabiwa au atachukuliwa kuwa yupo chini ya ulinzi halali iwapo:-

i) Atakuwa amezuiliwa kutokana na kosa, na kwamba afisa wa Polisi anaamini mtuhumiwa ametenda kosa au kosa linalolalamikiwa.

ii) Atakuwa amezuiliwa kutokana na kukamatwa kwake kihalali.

iii) Ikiwa afisa wa Polisi ataruhusiwa kumkamata kwa makosa yaliyoruhusiwa chini ya kifungu ha 14, cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai.

**NAMNA AU JINSI YA KUKAMATA**



Namna au jinsi ya kukamata imeainishwa chini ya kifungu cha 11(1), cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kwamba wakati wa kukamata afisa wa Polisi au mtu yeyote yule anayefanya ukamataji ni budi azingatie mambo yafuatayo:-

i) Ni lazima amguse bega au sehemu yoyote ya mwili wake mtu anayekamatwa.

ii) Ni lazima amjulishe mkamatwaji kosa lake mara moja, labda tu ithibitikek-

wamba mkamatwaji anafahamu kosa lake.

Kwa mujibu wa kifungu cha 11(2) cha sheria hiyo, mtu anayekamatwa ni lazima atii amri ya kukamatwa na asijaribu kukataa au kufanya fujo au kumshambulia afisa wa Polisi au kutoroka. Iwapo mtu anayekamatwa atakataa amri halali ya kukamatwa, au atafanya fujo kwa kumshambulia mkamataji au kujaribu kutoroka, sheria hii inamtaka mtu anayefanya ukamataji kutumia mbinu zozote ili kufanikisha ukamataji huo.

MATUMIZI YA NGUVU KATIKA KUFANIKISHA UKAMATAJI

Sheria inatilia maanani suala zima la kuepuka matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa ukamataji, kwamba ni jambo linalopaswa kuepukwa kwa kadri inavyowezekana. Lakini wapo **baadhi ya watu**, aidha **kwa makusudi** au kwa **kutokujua** wanaokaribisha **matumizi ya nguvu** dhidi yao, kwa kuruhusu hali au mazingira ya nguvu kutumika. Aheria hii inamtaka afisa wa Polisi au mtu anayefanya ukamataji atumie nguvu, tena ya kiasi tu pale inapolazimu.

Kifungu cha 21 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinafafanua matumizi ya nguvu katika kufanikisha ukamataji baada ya mbinu nyingi na sahihi kushindwa.

Kinaeleza wazi kwamba, iwapo mtu anayekamatwa atasababisha kujitokeza mazingira ambayo yatamfanya afisa wa Polisi au mtu anayetekeleza amri ya ukamataji ashindwe kufanya kazi hiyo, anaruhusiwa kisheria kutumia **nguvu ya kiasi** *(reasonable force),* dhidi ya mazingira yaliyojitokeza ili **kufanikisha ukamataji, kusuia shambulio au kuepusha utoro baada ya mtuhumiwa kukamatwa.**

Pia sheria inamwonya mkataji kutotenda kitendo chochote kitakachopelekea kutokea mauaji, aidha ya mtu anayekamtwa au mtu mwinguine.

Lakini sheria hiyohiyo inampa mamlaka na uwezo wa kuua pale ambapo afisa huyo atalazimika kufanya hivyo na kwamba anazo sababu za kuamini kwamba utendaji wa kitendo hicho ni wa lazima ili kukidhi mazingira yafuatayo.

i) Kuokoa maisha yake au maisha ya mtu au watu wengine.

ii) Kuzuia majeraha hatari *(serious injuries),* kwake yeye binafsi au kwa mtu au watu wengine.



**Tangazo**





Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com